

SURA YA KWANZA

UMUHIMU WA AMANI DUNIANI

Dunia inaweza kuwa na vitu vingi muhimu lakini amani ndiyo suala muhimu kuliko mambo mengine, ukweli nikuwa kwasasa dunia inakabiliwa na mambo mengi yenye kuipotenza tunu ya amani hii muhimu. Amani nikitu chenye ulazima kuhubiriwa kwawatu wote kwanini kwa watu wote? kwa sababu nisuala ambalo linamuhitaji kila mmoja, nijukumu la mtu yoyote yule duniani ambae anatakiwa kuishi ndani ya sayari hii ambayo ina taswira pana kuhusu suala hili.

Taswira ya kwanza ni umoja au watu kuwa wamoja, hii unaweza kuonekana kama umuhimu wa amani duniani kote tukiwa na amani na umoja kutapelekea utakuwepo mshikamano na maelewano. Amani ina nguvu katika kuwaleta watu pamoja nakuchukuliana kutokana na mapungufu watu walionayo kwenye mazingira ya kila siku, maelewano kati ya jamii moja na nyingine yanatokana na kuimarika kwa amani na ustawi wa uchumikunahitajika amani iwe ndani ya taifa kuwa na uchumi mzuri na ulio imarika inawezakana endapo amani itakuwepo.

Amani inaanza kwa mtu binafsi, kwanini inakuwa hivyo? tafiti kuhusu masuala ya amani inaonyesha ikiwa mtu mmoja atakuwa na wigo wakutenda mambo mazuri nakuyaepuka mambo yanayoweza kupelekea taswira mbaya katika jamii inanguvu kubwa ya kustawisha amani. Tunaposema amani haina maaana ya kundi kubwa la watu ama viongozi wanao ongoza watu wengine, laa hashu! amani inamgusa mtu mmoja mmoja. Mtu anaweza kuwa msimamizi na balozi wa kudumisha amani kuliko kundi kubwa la watu.

Unapo zungumzia amani kwa kumwangalia mtu nilazima kugusia matendo memaamabayo hayaanzi kwa kundi la watu huanza na mtu, matendo mema ni mjumuiko wa mambo mengi ikiwemo utii wa sheria bila kushurutishwa na hii ni sifa ya kwanza ya matendo mema. Mkanganyiko hutokea kutokana na mtu kutokuwa na utii wa sheria zilizowekwa, nilazima kutii mamlaka zilizoweka sheria juu ya mambo au mazingira ambayo jamii zinaishi. Hakuna maisha bila sheria hata vitabu vitakatifu vinaonyesha Mwenyezi Mungu alivyo uumba ulimwengu aliweka sharia.

Kufuata sheria katika utaratibu nikudumisha amani, ikianzia hasa kwa mtu mmoja au (binafsi) kutii sheria kuna maana pana, unapoitii sheria unatengeneza jamii ya watu wasikivu, jamii ya watu wenye heshima lakini unakuwa umetengeneza hali yakutokuwa na migogoro na watu. Pia unakuwa umesaidia mamlaka zilizoweka sheria kutoingia katika mivutano isiyokuwa na tija na watu au jamii.

Mwanajamii ninani? tafsiri inamaana kubwa katika kuelewa na kuelimisha, mwanajamii ambae anaye zungumziwa ni watu au mtu uwe kwenye mazingira yoyote uliopo wewe ni mwanajamii. Uwe katika hali ya chini au ya juu ni mwanajamii hivyo, jamii inaweza kuingia katika viashiria vya kutokuwa na amani kutokana tu na mtu mmoja peke yake hivyo hii inaweza kukupa uhalisia wa mtu binafsi kutunza amani. Kufuata